**KISWAHILI**
**KIDATO CHA PILI**
**MUHULA WA PILI 2025**
**MTIHANI WA MWANZO WA MUHULA**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

## UFAHAMU (ALAMA 10)

**Maswali**

a) Andika anwani inayofaa kifungu hiki (Ala. 1)

**Zaraa/kilimo**

b) Huku ukirejelea kifungu fafanua umuhimu wa kilimo hapa nchini (Ala. 2)

i) **Ni uti wa mgongo wa taifa**
ii) **Viwanda vingi hutegemea malighafi yake**
iii) **Huwalisha wafanyikazi**

c) Eleza changamoto tatu zinazowakabili wataalamu wa kilimo (Ala.3)

i) **Hawana usafiri**
ii) **Petroli ni kizungumkuti**
iii) **Ni wachache ikilinganishwa na wakulima wanaohitaji msaada wao**

d) Mbali na matatizo yanayowakumba wataalamu, onyesha matatizo mengine **matatu** yanayokumba sekta ya kilimo (Ala.3)

i) **ukosefu wa sera mwafaka kuhusu ardhi**
ii) **wananchi wengi huongozwa na taratibu za tamaduni**
iii) **kushindwa kwa mkulima kuongeza virutubishi ardhini**
iv) **mbolea huchangia uchafuzi wa mchanga**
v) **mabadiliko na hali ya anga**

e) Eleza maana ya msamiati ufuatao kulingana na kifungu (Ala.1)

Adimu - **Nadra / isiyo rahisi kupatikana**

## MATUMIZI YA LUGHA (Ala.30)

(a) Taja aina **mbili** za ala za sauti kisha utoe mfano mmoja mmoja (Ala.2)

i) **Ala tuli – mano, kaakaa gumu, kaa kaa laini, ufizi, koromoo**
ii) **Ala sogezi – midomo, ulimi**


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

(b) Taja maneno yenye miundo ifuatayo. (Ala.2)

**i)** KKKI **- nywa,mbwa,mpwa**

ii) Irabu pekee – **oa,ua,au**

(c) Taja njia **tatu** kuainisha konsonanti. (Ala.3)

**i) Mahali pa kutamkia/kubania sauti**
**ii) Namna ya kutamka**
**iii) Hali ya mghuno**

(d) Mofimu ni nini? (Ala.1)

**Ni sehemu ndogo zaidi ya neon yenye maana kisarufi na isiyoweza kugawika zaidi bila kupoteza maana.**

(e) Ainisha viambishi na mzizi kwenye neno lifuatalo. (Ala.3)

Hawakunichokoza

**Ha – kikanushi cha nafi**

**Wa – kiambishi cha nafsi ya tatu**

**Ku – kikanushi cha wakati uliopita**

**Ni – mtendwa**

**Chokoz - mzizi**

**A – kiishio**

**Ha-wa-ku-ni, chocoz – a**

**Vawali mzizi utamati**

(f) Yakinisha sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali timilifu. (Ala.2)

Msomi hakutuzwa siku hiyo

**Msomi atakua ametuzwa siku hiyo**

(g) Taja matumizi **mawili** ya alama ya mkwaju. (Ala.2)

**i) Kuongesha maneno yenye maana sawa mf. Tabibu/Daktari**

**ii) Hutuoa maana ya ama/au – utakula wali/sima?**

**iii) Kuandika tarehe 20/02/2012**

(h) Nyambua vitenzi vifuatavyo: (Ala.3)

i) Onja (kutendesha) – **Onjesha**

ii) Uza (kutendea) - **Uzia**

iii) Omba (kutendana) - **Ombana**


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

(i) Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi. (Ala.3)

Babu alimwambia mjukuu wake Fatuma aende alipokuwa

**"Fatuma, njoo hapa", babu alimwita mjukuu wake.**

**"Njoo hapa", Babu alimwita mjukuu wake Fatuma.**

(j) Maneno haya yamo kwenye ngeli gani? (Ala.2)

i) Mparachichi – **U - I**

ii) Manukato – **Ya - Ya**

(k) Kanusha sentensi ifuatayo (Ala.2)

Ningalifanya kazi nigalikuwa tajiri

**Nisingalifanya kazi nisingalikuwa tajiri**

(l) Bainisha maneno kwenye sentensi ifuatayo. (Ala.3)

Mvuvi amevua samaki wengi na mkulima

N T N V H N

.....................................................................................................................................

(m) Tunga sentensi **mbili** kwa kutumia vivumishi vionyeshi vya: (Ala.2)

i) Karibu – **mtoto huyu ameanguka vibaya**

**ii)** Mbali kidogo – **vitabu hivyo vimeangizwa kutoka mjini**

**(Mwalimu akadirie jibu la mwanafunzi)**

**ISIMU JAMII (Ala.5)**

(a) Eleza maana ya rejesta. (Ala.1)

**Ni matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali**

"Mwenda zake ameliacha pengo ambalo halitazibika haraka. Alikuwa muumini na mtanashati. Maulana……….

(Ala.1)

i) Tambua sajili hii.

**Mazishi/Matanga/Maombolezi**

ii) Eleza sifa za sajili hiii (Ala.3)


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

- ✓ **Sauti huwa ya chini**
- ✓ **Lugha ya huruma**
- ✓ **Lugha huwa ya majonzi**
- ✓ **Lugha hutia matumaini**
- ✓ **Lugha husifia mwenda zake**
- ✓ **Lugha huwa ya kuliwaza**

**FASIHI SIMULIZI (Ala.5)**

a) Eleza maana ya hadithi katika fasihi simulizi (Ala.1)

**Ni masimulizi yanayoeleza jambo la kweli au la kubuni kwa lugha ya mtiririko**

b) Taja dhima **nne** za hadithi katika jamii (Ala.4)

**i) Huburudisha jamii**
**ii) Huleta watu pamoja (hukuza umoja)**
**iii) Huonya dhidi ya tabia zisizokubalika**
**iv) Hufunza maadili yanayofaa kufuatwa na jamii**
**v) Huelekeza**
**vi) Huifadhi utamaduni wa jamii**
**vii) Hukuza lugha**
**viii) Hukuza ubunifu**

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes